## WMA YA MBARANG'ANDU

WMA ya Mbarang'andu ipo katika mkoa wa Ruvuma, kwa upande wa kaskazini inapakana na pori la akiba la Selous, na ni moja kati ya WMA tano zilizopo katika ushoroba wa Selous-Niassa. Ilisajiliwa mwaka 2006 na mwaka 2010 ilipata haki ya matumizi lakini iliendelea kuzalisha mapato ya uwindaji chini ya uangalizi wa seikali mpaka mwaka 2013. Mwaka 2013 asasi ya kiraia ya jumuiya ilipata umiliki wa kitalu cha uwindaji chini ya kanuni za WMA na hapo ilikuwa na uwezo wa kuchukua kiwango kikubwa cha mapato ya uwindaji ambayo hapo awali yalikuwa yakichuliwa na serikali kuu. Ina vijiji saba wanachana, ambavyo ni Kitanda, Nambecha, Likuyu Sekamaganga, Mchomoro, Kilimasera, Songambele na Mtelawamwahi, vyenye takribani ya wakazi 16,500 wa asili ya makabila ya wandendeuli na wayao. Wakazi wengi ni wakulima na baadhi hufanya kilimo cha kuhamahama, ingawa WMA imeweka vikwazo katika upatikanaji wa ardhi mpya kwa ajili ya kilimo. Kwa sasa, kuna mwekezaji mmoja katika uwindaji lakini hakuna wawekazaji katika utalii wa safari za kutizama wanyamapori.

## Kuhusu Mradi wa Utafiti wa PIMA

Utafiti wa faida na athari za Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) kwa mazingira na umaskini (PIMA) ni mradi wa utafiti wa kimataifa ulioendeshwa kwa ushirikiano kati ya Chuo Kikuu cha London, Chuo Kikuu cha Kopenihageni, Chuo Kikuu cha Imperial London, Chuo Kikuu cha Edinburgh, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania, Kituo cha Umoja wa Mataifa cha Ufuatiliaji wa Uhifadhi Duniani, na Jumuiko la Maliasili Tanzania. PIMA ilikusanya taarifa za ngazi ya kaya kuhusu mali na hali za kimaisha kwa kutumia madodoso na kwa kuzipanga kaya katika madaraja tofauti ya kipato. PIMA pia ilikusanya taarifa katika ngazi ya kijiji na WMA kuhusu uendeshaji wa WMA ikiwa ni pamoja na ugawanaji mapato. Taarifa hizi zilikusanywa katika vijiji 42 ndani na nje ya WMA sita zilizopo kaskazini na kusini mwa Tanzania. Upangaji wa kaya katika madaraja ya kipato ulifanyika kwa kaya zaidi ya 13,500. Dodoso lilitumika kukusanya taarifa kuhusu mali na mbinu za kujikimu kabla na baada ya kuanzishwa kwa WMA kutoka kwa wanaume na wanawake katika kaya zinazokaribia 2,000 (lengo ni kulinganisha hali ya maisha kati ya kipindi cha mwaka 2014-15 wakati wa utafiti wa PIMA na hali ilivyokuwa mwaka 2007 kulingana na kumbukumbu ya mhojiwa). Kwa kulinganisha mabadiliko ya hali ya maisha kabla na baada ya WMA kati ya vijiji vya WMA na vile visivyo vya WMA, athari za WMA kwa hali ya maisha zinaweza kujulikana (Kielelezo 2).

## Mapato ya WMA ya Mbarang'andu

- Mapato yatakanayo na tozo mbalimbali katika WMA yanapaswa kugagwanywa kulingana na Kanuni zinazosimamia Maeneo ya Jumuiya ya Wanyamapori za mwaka 2008 na 2012 (Kielelezo Na. 3).
- Mgawo wa mapato ya utalii hutolewa kwa serikali kuu (*nyeusi*) na kwa halmashauri ya wilaya *(nyeupe)*
- Mapato yanayobaki hurudishwa kwa asasi ya kiraia ya jumuiya inayosimamia WMA ambayo inaweza kubakiza nusu ya mapato *(michirizi)* na kugawanya nusu nyingine kwa vijiji wanachama (kijivu mpauko)
- Ripoti ya WWF ya mwaka 2014 inaonyesha kuwa mapato ya WMA kwa mwaka yalikuwa ni kati ya dola za kimarekani 2,800 na 22,700 kati ya mwaka 2008 na 2012. Mapato haya yalitokana na kitalu cha uwindaji kinachonendeshwa na serikali. Michango ya wafadhili kwa vijiji vya WMA, mwekazaji wa uwindaji wa kitalii na kampuni ya uchimbaji madini ulifikia dola za kimarekani 28,000 kwa 2012 na dola za kimarekani 33,000 kwa mwaka 2015. Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, vijiji vya Mbarang'andu vilipokea takribani dola za kimarekani 1,000 kwa mwaka, kutoka kwa asasi ya kiraia ya jumuaiya inayoendesha WMA

## Ramani ya WMA ya Mbarang'andu




**Kielelezo Na. 1: Ramani ya WMA ya Mbarang'andu (nyeupe). Kulingana na taarifa za kijiografia kutoka kwenye kumbukumbu za WWF. Imeandaliwa na J. Bluwstein**

## Fact box: Mbarang'andu WMA

| | |
|---|---|
| Wilaya | Rufiji |
| Vijiji Wanachama | 7 |
| Idadi ya Wakazi | 16,451 |
| Eneo | 2,900 $km^2$ |
| Mwaka wa usajili | 2006 |
| Jina la asasi ya kiraia | Mbarang'andu |




**Kielelezo Na. 1: Mbinu iliyotumiwa na PIMA kuonesha mabadiliko yaliyosababishwa na WMA**




**Kielelezo Na. 2: Mgawanyo wa mapato ya ada za uwindaji wa kitalii na utalii wa picha kulingana na Kanuni za Utalii wa Picha 2008 na Kanuni za Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori za Jamii za mwaka 2012.**

* WMA inaweza kufanya makubaliano ya kuongeza kiwango cha ada, ambapo 100% ya kiwango cha ziada hubakia kwa WMA. ** Ada kubwa kabisa kwa nyara hutozwa kwa aajili ya uwindaji wa Tembo: Kati ya dola za kimarekani 10,000 - 25,000, kutegemea na ukubwa wa meno ya Tembo. *** Hukusanywa na serikali kuu, na baadae kugawanywa kwa WMA baada ya kukatwa kodi. Ada hizi ni pamoja na ada ya mikataba, ada ya kulaza wageni, ada ya kutembea eneo la WMA, ada ya kuingiza gari n.k.

## Mabadiliko ya Hali ya Maisha katika WMA ya Mbarang'andu

### Mali

- Kulingana na mitazamo ya wakazi, kaya za Mbarang'andu zilipangwa katika makundi ya 'maskini sana' 'maskini' 'kawaida' na 'tajiri' kufuatana na kiwango cha mali kwa mwaka 2014 na kumbukumbu za umiliki mali kwa mwaka 2007
- Kwa wastani, kaya za Mbarang'andu zimejiongezea mali kati ya mawaka 2007 na 2014
- Ongezeko hili lilikuwa mara tatu zaidi katika vijiji vya WMA kuliko vijiji visivyo vya WMA
- Katika vijiji visivyo vya WMA, kaya nyingi zilibakia katika daraja la umiliki mali zilizokuwemo mwanzoni.
- Hata hivyo, hii haitokani na mapato ya WMA, kwa sababu hayakuwepo au yalikuwa kidogo sana. Noe (2013) anaonyesha kuwa michango ya 'marafiki wa Mbarang'andu' kutoka kwa asasi za uhifadhi na wachimbaji wa madini ya urani katika vijiji vya WMA iliweza kusaidia katika miradi Fulani




**Kielelezo Na. 4: Mabadiliko ya mali kati ya mwaka 2007 na 2014. Katika kila kaya 10 takribani 2.5 zilitajirika na 0.3 zilikuwa maskini katika maeneo yasiyo ya WMA. Katika maeneo ya WMA, takribani kaya 7 kati ya 10 zilitajirika na 0.2 zilikuwa maskini.**

### Upatikanaji wa Maliasili na Mapato yatokanayo na Mazingira

- Katika utafiti huu, upatikanaji wa maliasili maana yake ni kiwango ambacho sheria na kanuni huzuia au husaidia kaya kupata kuni, fito, asali ya porini, vyakula vya porini n.k. kwa ajili ya matumizi au biashara.
- Mapato yatokanayo na mazingira imaaminisha mapato yatokanayo na ukusanyaji na/au uuzaji wa maliasili.
- Utegemezi kwenye kuni na mboga na mtunda ya ya porini uliongezeka katika vijiji vya WMA na vile visivyo vya WMA, wakati mapato yatokanayo na vifaa vya kujengea, mbao, samaki, asali n.k. yalipungua kati ya mwaka 2007 na 2014 kulingansiha na mapato mengine ya kimazimgira (Kilelezo Na. 5)
- Mapato yatokanyo na samaki, asali, mbao na mkaa yanawakilisha mchango mdogo kwa maisha ya wanavijiji katika WMA (≤6%) na wale wasio katika WMA (≤3%)
- Upatikanaji wa rasimali nyingine za kimazingira umekuwa mgumu katika vijiji vya WMA, lakini ni wahojiwa wachache tu waliohusianisha ugumu huo na uwepo wa WMA




**Kielelezo Na.5: Mapato yatokanayo na rasimali za kmazingira katika vijiji vya WMA na vile visivyo vya WMA kwa mwaka 2007 na 2014.**

### Mbinu za Kimaisha

- Shughuli zinazoegemea katika mazingira (kama kilimo, ufugaji, mazao ya porini) zilichangia 83% ya mapato yote ya kaya za Mbarang'andu, na zile zisizo za WMA (Kielezo Na. 6). Mazao ya porini yanajumuisha kuni, vifaa vya kujengea, mbao, samaki, asali n.k
- Mchango wa kilimo, ufugaji, mazao ya porini na mapato kutokana na kazi za vibarua ulipungua katika kaya za WMA ya Mbarang'andu na zile zisizo za WMA kati ya 2007 na 2007 (Kielelezo Na. 7)
- Utegemezi katika misaada uliongezeka katika vijiji ya WMA na vile visivyo vya WMA kati ya mwaka 2007 na 2014 (Kielelezo Na. 7)




**Kielelezo Na. 6: Mchango (%) wa vyanzo mbalimbali kwenye pato la jumla (mwaka mzima) katika vijiji vya WMA ya Mbarang'andu na vile visivyo vya WMA kwa mwaka 2014**




**Kielelezo Na. 7: Mabadiliko ya mchango wa chanzo cha mapato kwa mwaka 2007-2014 kwa vijiji vya WMA na vile visivyo vya WMA**

**Ardhi ya Kilimo**

- Ardhi ya kilimo inapimwa kwa kulinganisha uwiano wa idadi na umri wa wanakaya, na inaripotiwa kwa kufuata uwiano wa ukubwa wa eneo na idadi ya watu wazima katika kaya yaani 'uwinano kwa mtu mzima' (AE)[1]
- Wakazi katika WMA, kwa wastani wana ardhi kubwa zaidi ya kilimo (kwa kipimo cha uwiano kwa mtu mzima) katika mwaka 2014 kuliko wakazi wa vijiji visivyo vya WMA (WMA: ekari 1.24 kwa mtu mzima, siyo WMA: ekari 0.95 kwa mtu mzima)
- Kwa vijiji vyote, yaani vile vya WMA na vile visivyo vya WMA, kumekuwa na mabdiliko kidogo kutokea mwaka 2007 kwenye wastani wa ardhi ya kilimo (kwa kipimo cha uwiano kwa mtu mzima)

**Ardhi ya Malisho**

- Nusu ya wahojiwa wote katika vijiji vya Mbarang'andu wanadhani kuwa upatikanaji wa ardhi ya malisho haujabalidika, na nusu wanadhani kuwa umekuwa mgumu sana, hata hivo siyo kwa sababu ya WMA
- Majibu hayo ni sawa na yale ya vijiji visivyo vya WMA

**Mifugo**

- Neno 'mifugo' linamaanisha wanyama wote wafugwao majumbani. Ili kurahisisha ulinganishaji wa aina tofauti za wanyama na idadi (kama vile mbuzi, ndama na ng'ombe), PIMA inatumia kipimo kijulikancho kama 'kipimo cha mifugo'[2]
- Kati ya mwaka 2007 na 2014 idadi ya mifugo kwa kaya katika kijji cha Kitanda ilipungua kwa wastani wa kipimo cha mifugo 0.8, lakini haijabadilika au imeongezeka kidogo sana katika vijiji vingine vyote vya WMA na visivyo vya WMA
- Kaya zilizokuwa na mifugo michache (kwa kipimo cha mifugo) mwaka 2014 kuliko mwaka 2007 zilitaja mahitaji ya fedha kuwa ndio sababu ya kupungua kwa mifugo

## Athari za Wanyamapori kwa Wakazi wa vijiji vya WMA ya Mbarang'andu

- Athari za wanayamapori kwa wakazi ni pamoja na vifo na majeraha kwa binadamu na mifugo, uharibifu wa mazao na mali nyingine. Matukio haya husababisha hasara kubwa.
- Kwa wastani, kaya 6.5 kati ya 10 katika vijiji vya WMA zilikumbwa na uharibifu wa mazao kutokana na uvamizi wa wanyamapori mashambani katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, kulinganisha na kaya 3.5 kati ya 10 katika vijiji visivyo vya WMA (Kielelezo Na. 8)
- Kuna utofauti mkubwa wa uwiano wa kaya zilizokumbukwa na uharibifu wa mazao katika vijiji vya WMA ya Mbarang'andu katika kipindi cha miezi 12 iliyopita (Kielelezo Na. 8)
- Kwa wastani, wahojiwa katika vijiji vya WMA na vile visivyo vya WMA waliripoti kuwa viwango vya uhabrifu wa mazao havijabadilika tangu 2007
- Wastani wa hasara ya mazao katika kipindi cha miezi 12 iliyopita ni mkubwa zaidi katika vijiji vya WMA kuliko vijiji visivyo vya WMA (Kielelezo Na. 9)




**Kielelezo Na. 8: Wastani wa uwiano wa kaya za WMA (66%) na zisizo za WMA (36%) zilizokumbwa na uharibifu wa mazao kutokana na uvamizi wa wanyamapori mshambani katika kipindi cha miezi 12 kabla ya utafiti.**




**Kielelezo Na. 9: Wastani wa hasara iliyotokana na uharibifu wa mazao kwa kaya katika vijiji vya WMA na visivyo vya WMA. Angalizo: Kiwango cha hasara kimekokotolewa kutokana na makadirio ya eneo lililoharibiwa, uzalishaji wa mazao, na makadirio ya pesa za mauzo ya mazao**

## Hitimisho




**Kielelezo Na. 10: Kijiji cha Kilimasera. Picha na J. Bluwstein**

Takwimu za madaraja ya umiliki wa mali zinaonesha kulikuwa na maendeleo chanya katika vijiji vya WMA ikilinganishwa na vijiji visivyo vya WMA. Hata hivo, hatuwezi kuhusianisha maendeleo hayo na mapato ya WMA kwa kuwa kihistoria, kabla ya kuanzishwa WMA, kulikuwa na mtiririko wa mapato katika vijiji vya Mbarang'andu kutoka katika mpango wa pori la akiba la Selous wa miaka ya 1990 na vitalu vya uwindaji vinavoendeshwa na serikali, pamoja na shuguli za uchimbaji madini katika eneo hili. Serikali kuu iligawana sehemu ya mapato ya uwindaji na jamii, wakati wawindaji, wachimbaji wa madini na asasi zisizo za kiserikali za uhifadhi mara kwa mara zilichangia fedha ili kuhakikisha mahusiano mazuri na jamii inayowazunguka (Noe 2013). Ni pale tu utafiti wa PIMA ulipokuwa unaelekea ukingoni, ndio WMA ilianza kuzalisha mapato yake yenyewe, hata hivyo, kwa kiwango kidogo. WMA yenyewe haionekani kuwa na mchango katika mabadiliko ya wastani wa ardhi ya kilimo. Upatikanaji wa vifaa vya kujengea ulikuwa mgumu zaidi, wakati upatikanaji wa kuni uliboreka zaidi katika vijiji vyote, yaani vijiji vya WMA na vile visivyo vya WMA. Tatizo la uharibifu wa mazao ni kubwa kwa vijiji vya WMA, sababu kubwa inaweza kuwa ni ukaribu wao na pori la akiba la Selous ikilinganishwa na vijiji visivyo vya WMA. Tangu bunduki zilizokuwa zinamiliwa za wakazi zichukuliwe na serikali wakati wa operesheni Tokomeza mwishoni mwa 2013, watu wamekosa uwezo wa kujilinda wenyewe dhidi ya tembo wnaoharibu mazao, kama walivyokuwa wanafanya kabla kwa kurusha risasi hewani. Ukaribu na pori la akiba la Selous unafanya ulinzi maalumu kuwa muhimu kwa ajili ya kulinda mazao ya wakulima, lakini WMA haiwezi kufanikisha hilo mpaka pale suala hilo litakapofanywa kuwa ndio kipaumbele cha walinzi wa WMA na WMA kuzalisha mapato makubwa ili kuwafidia watu kutokana na hasara zitokanazo na wanyamapori waharibifu. Tuna mashaka makubwa kama WMA ya Mbarang'andu na WMA nyingine katika ushoroba wa Selous-Niassa zinaweza kuvutia uwindaji wa kitalii au utalii wa kutizama wanyamapori ili kuzalisha aina ya mapato yanayohitajika angalau kufidia hasara zinazowakabili wanajamii katika WMA kutokana na uharibifu wa mazao na hasara zinazotarajiwa baadae kutokana na vikwazo katika upatikanaji wa rasilimali na ardhi ya kilimo. Wasiwasi mwingine kuhusu jamii ya WMA ya Mbarang'andu ni uwindaji haramu kwa ajili ya nyama. Uwindaji kwa wakazi uliahidiwa kama faida ya kuwa sehemu ya WMA, hata hivyo, tangia mwaka 2012, idara ya wanyamapori haijawahi kutoa sehemu ya wanyamapori kwa ajili ya uwindaji wa wakazi, kitu ambacho hakichochei mtizamo chanya kwa WMA

## Kumbumbuku Rejea

[1]Katika matokeo haya, ardhi ya kilimo imeainishwa na idadi ya watu katika kaya, jinsia na umri, kwa sababu wanaume, wanawake, na watoto wa umri tofauti huhitaji kiwango tofauti cha chakula, na hivyo ukubwa sawa wa ardhi humaanisha uwezo tofauti wa kutosheleza mahitaji kwa kaya mbalimbali. Kwa kutumia mfumo sanifu, tunawajumlisha wanakaya na kuwaweka katika kipimo cha 'uwiano wa mtu mzima' (AE), ambacho ni rahisi kulinganisha umiliki wa ardhi ya kilimo na mahitaji kwa kaya

[2] Kama ambavyo PIMA imetumia mfumo sanifu wa uwiano wa mtu mzima (AE), tunatumia 'kipimo cha mifugo' ili iwe rahisi kulinganisha makundi ya mifugo yanayoundwa kwa aina na ukubwa tofauti wa mifugo na mahitaji yao tofauti ya chakula. Kipimo kimoja cha mfugo ni sawa na ng'ombe mmoja mkubwa wa kilo 250kg. Mbuzi au kondoo kwa mfano, anahesabiwa kuwa sawa na moja ya kumi ya ng'ombe.

## Shukrani

PIMA inawashukuru wakazi wa vijiji vya Kitanda, Nambecha, Kilimasera, Songambele, Mputa, Naikezi, Chengena, na Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Mbarangandu kwa kushiriki katika utafiti huu. Mradi wa utafiti wa PIMA umefadhiliwa na ESPA: Mpango wa Utafiti wa Mazingira na Kuondoa Umaskini. ESPA inaendeshwa kwa pamoja na Shirika la Misaada ya Kimataifa la Uingereza (DFID), Baraza la utafiti wa Mazingira (NERC) na Baraza la Utafiti wa Uchumi na Jamii (ESRC). Kwa maelezo zaidi tembelea tovuti hii:
www.ucl.ac.uk/pima

Jarida hili limeandaliwa na S. Funk kutokana na takwimu zilizokusanywa na mradi wa utafiti wa PIMA. A. Keane, M. Reinhardt Nielsen, J. Friis Lund, J. Bluwstein and K. Homewood kwa pamoja waliandaa mbinu za kukusanya, kuchambua na kutafsiri takwimu za PIMA. J. Olila aliongoza kikundi cha wakusanya takwimu. M. Msuha and N. Burgess walihusika na takwimu za wanyamapori.

## References

Noe, C (2013): Contesting village land: uranium and sport hunting in Mbarang'andu Wildlife Management Area, Tanzania. *Journal of Utafiti*, 10(1) 39-60

Kangalawe, R.Y.M and Noe, C (2012): Biodiversity Conservation and Poverty Alleviation in Namtumbo District, Tanzania. *Journal of Agriculture, Ecosystems and Environment*, 162(1)90– 100

WWF (2014): Tanzania's Wildlife Management Areas, 2012 Status Report.

**Mawasiliano:** K. Homewood, Chuo Kikuu cha London, Idara ya Anthropologia. k.homewood@ucl.ac.uk